**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

143 Barabara ya Julius Kambarage Nyerere
Mazizini, S.L.P 394
70475 Mjini Magharibi, Zanzibar

Tovuti: www.moez.go.tz
Barua pepe: info@moez.go.tz

**12 FEBRUARY, 2026.**

# TANGAZO MAALUMU.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar inapenda kuwataarifu Wazazi, Walezi na Wahitimu wa Kidato cha nne, Kidato cha sita na Vyuo vya Kati wanaokusudia kuendelea na masomo yao ya Elimu ya Juu nje ya Nchi kuwa kabla ya kufunga mkataba na Wakala wa Usafirishaji Wanafunzi Kimasomo Nje ya Nchi wanashauriwa kufika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali **chumba namba 57** katika Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu ili kuthibitishiwa uhalali wa Wakala wanaemtaka kumtumia.

**Aidha,** Jamii inakumbushwa kuchukuwa tahadhari kutokana na kuibuka kwa Wakala ambao **sio Waaminifu** wanaosafirisha Wanafunzi Nje ya Nchi kwa kuwaahidi kuwapatia Vyuo pamoja na huduma nyengine.

Wizara inawaasa Umma kuwa wasikubali kauli ya Wakala yeyote kabla ya kupata ithibati ya Wizara ili kuepusha malalamiko yanayoweza kuepukika.

Ili kujua orodha ya wakala waliothibishwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (**TCU**) kusafirisha wanafunzi nje ya nchi kwa mwaka 2025/2026, tafadhali tembelea kiungo (link) kifuatacho.

https://share.google/0K7x8HWMOXA83BebM.

Ahsante,

Imetolewa

Kitengo cha Habari na Mawasiliano,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
**Zanzibar.**

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
P.O. Box 394
ZANZIBAR